# UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Simu: +(257) 22 248636**
**Nukushi : +(257) 22 248637**
**Barua pepe: tanzanrep@usan-bu.net**

**Kinindo**
**Avenue Du Large,**
**Nyumba namba. 51,**
**S.L.P 855,**
**BUJUMBURA,**
**BURUNDI.**

***Unapojibu tafadhali taja:***

**Kumb.Na. CHAB 357/448/01/35**

**15 Aprili, 2020**

Watanzania wote Waishio nchini Burundi,

KUH: **SERIKALI YA TANZANIA YASIMAMISHA SAFARI ZOTE ZA NDEGE ZA ABIRIA ZA KIMATAIFA NA ZA KUKODI KUINGIA NCHINI TANZANIA KAMA HATUA MOJA WAPO YA KUKABILIANA NA UGONJWA WA COVID-19**

Baada ya kupitia upya hali ya ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID-19) unaosababishwa na virusi vya Corona katika bara la Afrika na duniani kwa ujumla, serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeamua kusimamisha safari zote za ndege za abiria za kimataifa na ndege za kukodi kuingia Tanzania kuanzia tarehe 11 Aprili, 2020 kama hatua mpya katika kukabiliana na ugonjwa wa COVID-19.

Ndugu watanzania muishio nchini Burundi, Ubalozi unawakumbusha kuendelea kuchukua tahadhali dhidi ya ugonjwa huo hatari, huku mkifuata maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Afya ya Burundi.

Aidha, kila mmoja kwa imani yake, tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu atuepushe na janga hili.

Ubalozi unashukuru kwa ushirikiano wenu.

Dkt. Edmund J. Kitokezi

Kny **BALOZI**